

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),

S.L.P 02,

USHIROMBO,

BUKOMBE.

**MKOA WA GEITA:**

**Simu:** 028 2520709

**Barua Pepe:** [ded@bukombedc.go.tz](mailto:ded@bukombedc.go.tz)

**Tovuti:** [www.bukombedc.go.tz](http://www.bukombedc.go.tz)



## **TANGAZO KWA UMMA.**

### **BEI ELEKEZI YA MBOLEA WILAYANI BUKOMBE.**

Katika kutekeleza azma ya Serikali ya awamu ya tano ya kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda ifikao mwaka 2025, juhudi kubwa imefanyika ili kutimiza malengo ya kimkakati kuelekea kilimo cha biashara na moja ya mikakati ni kuhakikisha mkulima anapata pembejeo za kilimo hususani mbegu bora, mbolea na viwatilifu kwa bei iliyohalalishwa. Kwa mujibu wa sheria, mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania (TRFA) imetangaza bei elekezi kwa mbolea za kupandia (DAP) na mbolea ya kukuzia (UREA).

Kwa wilaya ya Bukombe bei elekezi itakuwa ni Tsh.54,987 kwa mbolea ya kupandia na Tsh. 42,408 kwa mbolea ya kukuzia bei hizi zimeanza kutumika tangu tarehe 15/09/2017 ilipotangazwa na Waziri wenye dhamana kwa nchi nzima.

Aidha bei za mbolea hizi zimepangwa kwa kuzingatia umbali na aina ya usafiri unaotumika na bei hii inayotangazwa ni hadi kwenye duka la muuzaji wa rejareja.

Ili kutekeleza mikakati hiyo, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana nawadau wake ilifanya marekebisho ya kanuni za mbolea za mwaka 2011 kupitia The Fertilizer (Amendment) Regulatory, 2017 ambayo moja ya marekebisho hayo ni kuhakikisha bei ya mbolea inadhibitiwa kwa kutoa bei elekezi.

Imetolewa na:

Kitengo cha Teknolojia, Habari na Mawasiliano.

Oktoba 4, 2017

**BUKOMBE.**